

Mafundisho maalumu kwa wanandoa - Wanawake.

Ikiwa utapenda kupata mafundisho mengine ya namna hii, basi fungua link hii uweze kuyasoma. >>.

<https://wingulamashahidi.org/category/mafundisho-ya-wanandoa/>

Habari ya Samsoni na Delila inafundisho kubwa nyuma yake kwa wanandoa. Wengi wanafikiri Delila alikuwa mwanamke kahaba ambaye Samsoni alimuokota tu na kukutana naye. Lakini uhalisia ni kwamba Delila alikuwa ni mke wa Samsoni.

Lakini mwanamke huyu, aliweza kubadilishwa akili kwa tamaa tu ya fedha. Ni mwanamke ambaye alipendwa sana na Samsoni, chochote ambacho angetaka kwa Samsoni angepatiwa. Lakini Wafilisti walipoona mwenendo wa Samsoni jinsi alivyompenda sana mwanamke huyu. Wakatumia fursa ile, kumshawishi Delila, kwa kumuahidia donge kubwa la fedha. Ili tu atoe siri ya asili ya nguvu zake.

Delila, akakubali, akaanza kumshawishi Samsoni, kwa kipindi kirefu, na hatimaye akafunuliwa siri ya nguvu zake. Akaenda akaziuza kwa wafilisti, kwa vipande vya fedha.

Waamuzi 16:4 Ikawa baada ya hayo akampenda mwanamke mmoja katika bonde la Soreki, jina lake akiitwa Delila.

5 Nao wakuu wa Wafilisti wakamwendea, wakamwambia, Mbembeleze, upate kujua asili ya nguvu zake nyingi, na jinsi tutakavyoweza kumshinda, tupate kumfunga na kumtesa; nasi tutakupa kila mtu fedha elfu na mia moja.

6 Delila akamwambia Samsoni, Tafadhali uniambie asili ya nguvu zako nyingi, na jinsi uwezavyo kufungwa, ili uteswe.

Kama mke, upendo wako unapohamia kwenye fedha, ni dalili madhubuti kuwa unaua nguvu ya ndoa yako (ambayo ipo kwa mume). Usitangulize mali mbele ya ndoa yako, wala usishawishiwe na fedha kwa chochote ukadharau thamani ya mumeo. Samsoni hakuwa mfanya biashara au mwajiriwa wa kampuni Fulani, hakuwa hata na akaunti benki. Lakini alikuwa mwamuzi wa Taifa teule la Mungu. Mtetezi wa wanyonge, na mkombozi wa walioonewa, hakujitajirisha yeye, alilitajirisha taifa,. Jambo ambalo Delila hakulithamini. Akawa tayari kuoielewa na fedha(wafilisti) na sio nguvu zake(Samsoni).

Leo wapo wamama, ambao wanachotafuta kwa waume zao ni fedha tu, fedha tu, fedha tu.. wakikosa hiyo wapo tayari kufanya chochote. Wengine hata kuanzisha mahusiano na watu wengine wenye uwezo wa juu, hawajua kuwa mwanaume anaweza asiwe tajiri kifedha, lakini ana nguvu za kuiendesha na kuilinda familia yako, jamii yako, ndugu zako, kipawa alichonacho kikaweza kukufanya wewe ukae vizuri au kuistaajibisha jamii au taifa, Lakini endapo tu utakiona hicho na kukithamini ndani yake.

Hivyo, kama mwanamke, toa moyo wako hapo kabisa.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kupenda fedha kutaibomoa ndoa yako.

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

<https://wingulamashahidi.org/category/mafundisho-ya-wanandoa/>

Mtande ni nini? Ni funzo gani lipo nyuma yake?

KITENDAWILI CHA SAMSONI

Je! mtu anapofunga kwa muda wa SAA 24, anapaswa kunywa maji au kitu chochote?

Kupenda fedha kutaibomoa ndoa yako.

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp